**“Utumaji Wa Meseji Za Ngono”, Tatizo Jipya Kwa Wakristo.**

Kabla hujaisoma blogu hii, tafadhari fahamu kwamba inajumuisha mafundisho ambayo wengine wangeyaita “mafundisho makomavu”. Ingawa yaweza kusemwa hivyo, tunalozingatia ni lile ambalo sote tunatakiwa kulitafakali kwa makini! Pia, tafadhari fahamu kuwa, naliandika makala hii siku kumi zilizopita, na nikaketi kitako kulitafakari jambo hili kwa undani.

Nadhani kiutamaduni, nimekuwa mshamba na mwenye mawazo ya kijima. Sijawahi kulisikia neno “meseji za ngono” hadi mwezi uliopita kama sikosei, au kama nimewahi kulisikia huko nyuma, sikulitilia maanani hata kidogo. Kama nilivyosema, kiutamaduni mimi ni mshamba na mwenye mawazo ya kijima na ikanilazimu kuingia mtandaoni kwa ajili tu ya kuhakiki kama nilikuwa nalitamka vizuri neno lenyewe. Tangu nimejua maana ya “meseji za ngono”, ni kama kila ninapokuwa natafuta habari mpya, nasikia “meseji za ngono, meseji za ngono, na meseji za ngono zaidi”. Kwa njia ya blogu hii, napenda kukushirikisha mawazo kadha wa kadha muhimu kwetu tunaotaka kumpendeza Mungu maishani mwetu.

Kwanza, hebu nitoe fafanuzi halisi ya “meseji za ngono” kama nilivyopewa na rafiki zangu katika Kristo ambao wana ufahamu mambo haya zaidi kuliko mimi. Nimeambiwa humaanisha “kushawishi, kutongoza hadi kufikia lengo, na au kutuma jumbe na picha zinazochochea ngono.” Pia, nimeambiwa kuwa neno lenyewe limetumiwa kiholela na wengine, wakati pengine neno lingine lingepaswa kutumiwa wakati wa kujadili utumaji wa aina fulani za jumbe ambazo si za ngono kwa asili yake. Hata hivyo, ngono ni ngono tu bila kujari tunaiitaje. Labda Bill Clinton hakujua ngono ni nini, lakini wengi wetu wenye umri zaidi ya miaka nane tunajua.

Pili, ni aibu leo kuona maendeleo ya kiteknolojia yanaharibiwa na dhambi. Kutumiana ujumbe ni maendeleo ya ajabu yanayotamba kwa miaka michache tu, na kufanya mawasiliano yawe rahisi mno. Lakini kama ilivyo kwa kila chema ulimwenguni, mungu wa dunia hii (2 Wakorintho 4:4), anapata fursa ya kuyatumia maendeleo hayo kwa manufaa yake.

Tatu, karibu kila mtu amesikia kashfa mpya ambayo imemtokea mbunge wa bunge la wawakilishi kule New York. Huyu jamaa ameoa mwanamke mzuri ambaye sasa hivi ana mimba. Siku kadha zilizopita imebainika kwamba amekuwa akituma meseji za ngono kwa wanawake tofautitofauti kwa miaka mingi hata wakati wote wa ndoa yao ambayo ina muda mfupi.

Kwa muda wa juma zima sasa, kashfa hii imeteka mashirika ya habari. "Simu baada ya simu zinapigwa" kutoka kwa wanachama wa kila chama cha kisiasa wakimtaka ajiuzuru. Na kila wakati amekuwa akiyapuuza hayo madai kwa ukaidi. Kama anajiuzuru au hajiuzuru, tutaona.

Nne, vipi kuhusu kashfa hii? Imekukera? Hivi hii tabia unaiona ni njema, yenye haki na safi? Watu wanapowatumia wengine picha za uchi, kutuma ujumbe na kutongazana, hili ni jambo la kusifia? Hivi, inakukera kuona mtu aliyeoa anafanya hivi? Je, inakukera kuona mtu anayewakilisha wananchi anatumia muda wake mwingi kutuma meseji za ngono? Endapo umekereka na kuchukizwa kwa kile ambacho amekuwa akikifanya, basi wewe ni sehemu ya ambacho wengine wanachelea kuwa. Watu waishio vijijini katika nchi hii ambao ni wakristo waaminifu…" na"…kiutamaduni…ni washamba."[1]

Naona fahari kuwa na Biblia na kujitahidi kuyaishi mausia yake, Zaburi 119;9-16. Naona fahari kusema kuwa ndoa ni baina ya mume na mke, Mathayo 19:4-6. Naona fahari kutambua kuwa uzinzi ni dhambi, Wagalatia 5:19-21. Naona fahari kusema kuwa "kitanda cha ndoa" ni "kitanda" pekee ambacho si najisi , Waebrania 13:4. Naona fahari kusema kuwa mwanaume yeyote anayempita chini mkewe ni tapeli hasa wakati ambapo mkewe ana mimba yake!Na kama hayo yananifanya niwe "mshamba mwenye mawazo ya kijima," basi nichukulie kama " mshamba" huku nikiwa na chale mabegani mwangu! Mungu aiokoe Marekani, kwa sababu tunaitaka!

Tano, Meseji za ngono ni dhambi? (unaposoma hapa zingatia fafanuzi iliyotolewa hapo juu.) Tafadhari zingatia yafuatayo (hata hivyo, najua zipo fikra nyingi ambazo ningetaja.):

1) Mpango wa Mungu ni kwamba vijana wanatakiwa kusubiri hadi waoane ndipo waanze ngono, Mwanzo 2:23-25; Warumi 1:29, etc. Na hawa vijana , na hata watu wazima wanaoshiriki kutuma meseji za ngono wanapaswa kujua kabisa kuwa utumaji wa mesei za ngono ni ngono najisi, upotofu wa kingono, ngono chafu na wote wafanyao mambo ya jinsi hiyo wana hatia ya uasherati. Asiwepo mwana wa Mungu anayefanya uchafu huu. “Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu” Mathayo 5:48
2) Kulingana na hali ya watu ambao hawako kwenye ndoa, maneno na picha chafu huamsha hamu ambayo haitakiwi kutulizwa isipokuwa ndani ya ndoa. Tafakari kwa makini maneno haya yaliyosemwa na Sulemani Wimbo ulio bora “Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vema yenyewe. 2:7; 3:3:5; 8:4. Najua kuwa wanasomi wa maandiko wamegawanyika kuhusiana na maana hasa ya maneno haya. Wengine wanasema maneno haya yanamaanisha kuamsha ashki kabla ya wakati upasao. Wengine wanasema kuwa maneno hayo yanamaanisha kuwa “usiwaache wengine wakakuingilia kwenye njozi ya mapenzi”. Vyovyote iwavyo, la kuzingatia ni lilelile- kuna wakati wa ndoa. “Penzi komavu”. Meseji za ngono zaweza kuwaghiribu vijana (na watu wazima pia) kutenda yasiyopasa kabla haujawa wakati muafaka.
3) Meseji za ngono ni kichocheo cha tamaa za ujanani, na hufanywa na wale wasio na mioyo safi kabisa. Mtume Paulo alimwagiza Timotheo “ Lakini zikimbie tama za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi “ 2Timotheo 2:22
4) Meseji za ngono kwa wenye umri chini ya miaka 18 ni kinyume cha sheria, Warumi 13:1ff, na wana wa Mungu wote wanapaswa kuzitii vilivyo sheria za nchi.
5) Meseji za ngono ni dhambi kwa sababu ni kitendo kinachokiuka mtazamo wa adabu na ungamo la uchaji Mungu. Tena, angalia Mtume Paulo alichomuagiza Timotheo, “ Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kuisitiri, pamoa na adabu nzuri…….kama iwapasavyo wanawake wanaukiri uchaji wa Mungu“ 1 Timotheo 2:9-10

6) Utumaji wa meseji za ngono ni tatizo kwa mwanadamu kwa sababu wale wanaotaka kuridhisha hamu zao kwa hakika watakumbana na ghadhabu ya Mungu, Warumi 13:4.
7) Utumaji wa meseji za ngono ni dhambi kwa sababu maneno yetu yanatakiwa “yakolee munyu” ili kuitegemeza roho inayonyong’onyea, badala ya lugha chafu inayotumika mara kwa mara wakati wa kutuma hizo meseji, Wakolosai 4:6; Waefeso 4:29; 1 Wathesalonike 5:11.
8) Kutuma meseji za ngono ni dhambi kwa sababu mtu anakuwa anapanda kwa mwili, Wagalatia 6:7. Katika hali hiyo watavuna kwa kadri ya walichopanda. Wengi walioituma picha za uchi wao, siku moa watajuta. Wanapokuta picha hizi ziko mtandaoni, milele na milele haitotokea kusema basi. Itakuwa aibu, unapopoteza fursa za ajira, familia yako inapojikwaa juu picha hizo, au hata pale ambapo mmoja wa wanao siku moja atakaozikuta hizo picha mtandaoni! Ikitokea, aibu na huzuni vitatanda kila pahala. Lakini kumbuka, Mungu alionya “unavuna upandacho” Mithali 4:24-26.
9) Utumaji wa meseji za ngono ni uovu, kwa sababu “Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema” 1 Wakorintho 15:33. Hivi ni wangapi wataharibiwa na meseji za ngono kabla hawajazinduka?
10) Pamoja na haya yote, hebu tutafakari swali hili muhimu; uzinzi wa kutuma meseji za ngono unatoa mazingira ya talaka? Wafilipi 4:8 yatufundisha “yatafakarini hayo” Je, mtu mtauwa na wa maana angedumu katika mambo yapi? Dhahiri, kutokana na maneno ya Paulo, tumeona ulazima wa kuzingatia kwa makini mambo ambayo ni “ya kweli, ya staha, ya haki, yaliyo safi, yenye kupendeza, yenye sifa njema” tunapotafuta kumpendeza Mungu.

Katika Mathayo 5:27-29 Yesu alisema “ mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake,” mst. 28. Utumaji wa meseji za ngono ukiishafanyika, na jambo hilo likienda bila kutubu, mtu aliyetenda hayo anakuwa anaelekea Jehanamu, mst. 29. kukosekana kwa maneno huu mstari “uzinzi wa kifikra” . Huo uzinzi wa kifikra ni zaidi ya kupepesa macho kwa mrembo. Hujumuisha mengi zaidi ya kuutambua uzuri wa mtu. Neno la asili la “tamaa” humaanisha kuona hamu, kufikiria, kutaka mno”. Neno hilo hilo

lililotumika katika Luka 15:16 na 16:21 kwa habari a mwana mpotevu na ombaomba, aliyekuwa na njaa hata “akatamani” makombo na chakula cha nguruwe ili ale. Neno la asili huhusisha zaidi ya kumpepesa, au kutazama na kuutambua uzuri. Kwa maana hiyo huhusisha hamu ya ndani juu ya kitu ambacho mtu hana haki nacho. Mawazo ya ngono yaliyopindukia namna hii ndiyo yampelekeayo mtu kutenda dhambi ya uzinzi wa moyoni, na inapotokea hali hiyo imeendekezwa mtu huyu huwa tayari kutenda kitendo chenyewe.

Pamoja na haya yote, tunakabiliwa na swali “Je, kutamani, au ‘uzinzi wa kififkra’ hutoa mazingira ya talaka kulingana na Mathayo 19:9? Mambo kadhaa yanapaswa kuzingatiwa ili kuona ukweli wa hili.

Kwanza, tamaa ni jaribu linalomfanya mtu “kuvutwa”, ambapo ni wazi kuwa matokeo yatakuwa ni dhambi, asipoikimbia zinaa 1 Wakorintho 6:18. vitendo hivi ni matokeo ya moyo ulio mahali pasipopasa, Wakolosai 3:2, matokeo yake ni dhambi.

Pili, mtu anaweza kujaribiwa na moyo na asifikie matashi ya mwili, 1 Wakorintho 10:12,13. Yesu “alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote bila kufanya dhambi”, Waebrania 4:15. Si kila jaribu hutupelekea kwenye dhambini.

Yakobo anazungumzia jaribu linavyoweza kutupeleka kwenye tamaa na ushawishi,na tamaa ikiisha kutunga mimba “huzaa dhambi,” Yakobo 1:14-15. Hivyo, mtu anaweza kutamani, na kutenda dhambi kwa kung’ang’ania kuwaza yasiyofaa (Wakolosai 3:1-2), lakini akawa hajawa hajaenda mbele hadi kuwa uhusiano wa kimwili jambo ambalo hupelekea malazi ya ndoa kuwa najisi, Waebrania 13:4.

Elewa kwamba utumaji wa “ meseji za ngono” kwa kawaida humaanisha kushawishi, kutongoza, kuamsha hamu, kwa kutumia jumbe na picha za uchi” na bado kuna kiwango kingine kwa wengine, pale ambapo kusudi la kutuma meseji za ngono kwa wasio wenza wao (mathalani, kufanya mapenzi kwa simu), ni kutimiza matamanio ya mwili. Mtu anapofanya hivi, ni uasherati.

Kwenye kisa nilichotaja hapo juu, wanaojihusisha na hayo wamechagua kumruhusu mtu mwingine kuingia kwenye hisia, mwili, na mahusiano ya

kimapenzi ya pingu za maisha, ili kuyaridhisha matamanio ya kimwili. Ikiwa ni kwenye chumba kingine, jengo, Nchi, jimbo, ni yale yale. Ingawa hawa wawili watakuwa wametenganishwa na umbali, bado watakuwa wameingia kwenye kile kinachowatuliza matamanio kwa mmojawapo au wote. Kwa kadri hilo linavyoendelea, endapo mmojawapo ameoa/kuolewa au wote bado malazi ya ndoa zao yanakuwa **najisi**, Waebrania 13:4. Kama wote hawajao/kuolewa, basi uasherati unakuwa umefayika.

Kama mwanandoa mmojwapo anatuma meseji za ngono kwa mtu mwingine, na tamaa ya ukaribu inazaa mahusiano na huyo mtu mwingine ambapo kuridhishwa kwa matamanio ya mwili kumetoka, huu ni uzinzi wa kivitendo? Bila shaka, ndiyo! Hivi tuseme "hapana", hicho kitendo tukiiteje basi? Ndiposa hiki kitendo kitoe mazingira ya talaka? Kwa mara nyingine, yawezekana, kama Yesu alivyosema katika Mathayo 19:3-9.

Shauku yangu siyo "kukifukunyua kiota cha manyigu" kwa haya niliyoandika, bali kuhimizana sisi kwa sisi, sote, wadogo kwa wakubwa, kwamba tuyatafakari kwa makini matendo yetu. Mungu hakukusudia kwamba tuishi kama mapaka pori! Tuutafute utakaso ambao angetaka tuwe nao.